

## BUKU LA 6

Salamu kwa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Kwa niaba ya Wilaya Shule za Kaunti ya DeKalb, ningependa kuwakaribisha rasmi wanafunzi na wafanyakazi kwa mwaka wa masomo wa 2020-2021! Nina furaha sana kuhusu mwaka huu masomo na ninatumaini kwamba pia wewe unafuraha. Iwe ni masomo ya ana kwa ana au ya mtandaoni, niko pamoja na wewe katika kuhakikisha uko katika njia sahihi ya kuwa tayari kwa kazi, masomo ya muda mrefu na ufanisi wa kielimu.

Wiki hii mada yetu ni ufanisi wa nyota tano. Ili wilaya yetu iweze kufanikiwa wakati wa nyakati hizi zenye changamoto, lazima tufanye kazi katika kiwango cha juu. Nilipata himizo nilipokuwa nikitembelea Mkoa wa Tano wiki hii - Shule ya Upili ya Martin Luther King, Jr., Shule ya Upili ya Miller Grove, na Shule ya Upili ya Southwest DeKalb ikiwemo shule za msingi na za kati. Nilikaribishwa vizuri na mpango kamili ambao uliangazia kwamba wanafunzi wetu wana msaada unaofaa wa kupaa juu na kufanikiwa. "Mkoa huu wa nyota tano" umefanya Ufanisi wa Wanafunzi kwa Usawa na Ufikiaji kuwa kipaumbele. Asante Mkoa wa Tano kwa kutoa mpango kamili wa mshikamano na data ya kuunga mkono mikakati na maono yenu.

Tunapoanza mwaka huu wa masomo, tukumbuke umuhimu wa Ufanisi wa Wanafunzi kwa Usawa na Ufikiaji. Lengo la 3 katika mpango wetu wa mkakati ni muhimu katika kuhifadhi ufikiaji wa elimu ya umma na ufanisi kwa wanafunzi wote wa DCSD, hasa wanafunzi ambao hawajawakilishwa vizuri. Nilishukuru Dkt. Weaver na timu yake kwa kutambua mianya, iwe ni ya kijiditali au ukosefu wa chakula, na kutambua suluhisho za kutuweka katika njia sahihi.

## UFANISI WA NYOTA 5 WA MKOA

Nilikuwa pia na fursa ya kukutana mtandaoni na viongozi wa kidini wa Kaunti ya DeKalb, Meya wa Dunwoody Lynn Deutsch na Kamishna Larry Johnson kujadili mahitaji na maslahi ya watoto wetu. Ilitia moyo pia kukutana na mawakili wa watoto, wanaoshiriki malengo na hoja sawa. Ninatazamia timu yetu ya Mahusiano ya Jamii ilete pamoja jamii zetu ili zifanye kazi kwa kushirikiana na kwa pamoja huku tukiwatetea wanafunzi wetu. Ninashukuru sana kwa michango na mwongozo wenu na ninajua Kwa Pamoja Tunaweza Kufanikiwa.

Tunapoanza kwa pamoja safari hii mpya na isiyo ya kawaida, ninataka nyinyi nyote muwe na maono akilini mwenu katika mwaka huu, hasa wakati mambo yanakuwa magumu. Ni ndoto ya wanafunzi wetu kuhitimu, kutabasamu katika kofia na gauni zao na wakiwa na hamu ya kukabiliana na ulimwengu. Baada ya haya yote, juhudi zetu zote zinapaswa kuangazia wakati huu na zaidi kwa kila mwanafunzi katika Kaunti ya DeKalb. Kama kawaida, asante kwa kazi yenu ngumu na kujitolea kwenu kwa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb. Kuweni na mwaka mwema wa masomo!

Shabiki wenu #1,

Cheryl Watson-Harris, Msimamizi

Shukrani maalum kwa Idara ya Kushirikisha Wazazi na Familia kwa kupanga mkutano wa mtandaoni wa Town Hall ambao unashughulika maslahi ya kijamii na kihisia ya familia zetu. COVID-19 imekuwa na kiwewe kwa familia zetu nyingi katika Kaunti ya DeKalb na duniani kote. Ikiwa ulikosa mkutano huu wa Town Hall, tafadhali bofya picha hii na utembelee ukurasa wa Facebook wa DSCD wa Kushirikisha Familia na ujifunze mengi kuhusu huduma za afya ya akili zinazotolewa na wilaya yetu.